


# UTAMBULISHO;



Habari za asubuhi kwako!

Nimeombwa niwatambulishe wanachama wa 'TEAM JESUS' wanaofanya kazi pamoja kuandaa na kutuma Africa Post kila wiki. Kwa hivyo wacha nianze Mwaka Mpya kwa kukuambia kidogo kuhusu sisi -- hasa kwa wale ambao bado hatujapata nafasi ya kukutana nao.

Timu yetu ilianza Machapisho ya Afrika takriban miezi saba iliyopita. Matumaini yetu ni kwamba baadhi ya mambo ambayo tumejifunza katika maisha, masomo, na huduma kwa miaka mingi yanaweza kuwa ya manufaa. Hivi sasa zaidi ya viongozi 500 wa Kikristo wanapokea Africa Post kila wiki.

Tupo wanne kwenye Timu. Mimi ni Doug Van Devender. Mimi huandika Machapisho kwa Kiingereza. Richard Cazzell hutayarisha Machapisho kwa ajili ya kuchapishwa na kuratibu na mtafsiri wetu wa Kiswahili "JK" nchini Kenya. Mtafsiri wetu nchini Rwanda, Noella, anasambaza Machapisho kwa lugha ya Kinyarwanda.

Richard na mimi tumekuwa tukifanya kazi pamoja katika huduma ya Afrika Mashariki tangu 1987. Kuanzia kwenye Pwani ya Kenya tuliendeleza uhusiano polepole kote nchini. Kadri ya miaka kumi na tano iliyopita tulianza kufanya kazi na wachungaji ambao ni marafiki wakubwa katika Wilaya ya Mara nchini Tanzania.

Agosti iliyopita, mimi na Richard pamoja na Dan Wessell, afisa mwingine wa Team Jesus, tuliwatembelea wachungaji marafiki nchini Kenya na Tanzania. Na kwa mara ya kwanza pia tuliwatembelea wachungaji marafiki nchini Rwanda kuhudumu nao wanaoongoza timu ya "Tunaenda Kwao" (WE GO TO THEM) yenye makao yake mjini Kigale.

Kwa pamoja Richard, Dan, na mimi tunasimamia huduma za mafunzo za Team Jesus Ministries Kimataifa.

Kuhusiana na mimi mwenyewe, Baba yangu alikuwa mkongwe wa Vita vya Pili vya Dunia. Yeye na mama yangu walifunga ndoa baada ya vita na kuingia huduma mara moja. Nina dada mmoja ambaye anampenda na kumtumikia Bwana.

Niliitikia wito wa Mungu kwa huduma nikiwa na umri wa miaka 18. Baada ya chuo kikuu nilikaa miaka miwili nchini Vietnam wakati wa vita katika huduma ya wanafunzi na kazi ya misaada ya wakimbizi huko Danang na Hue.

Baadaye mke wangu Betty na mimi tulioana tukiwahudumia wakimbizi wa Indochina baada ya vita. Tulihudumu kwa miaka miwili kisha tukahamia Mombasa, Kenya ambako tulikusanya timu ndogo ya uinjilisti na kwa pamoja tulianzisha makanisa manane mapya.

Baada ya kurudi Marekani, Betty na mimi tulijazwa na Roho Mtakatifu. Tulifunzwa katika huduma ya ROHO MTAKATIFU na mtumishi John Wimber huko California kisha tukaanzisha kanisa huko Fort Smith, Arkansas pamoja na Richard na mkewe Kathy Cazzell. Tulihudumu pamoja kwa miaka minane.

Baadaye tulitengeneza kielelezo chenye nguvu cha maombi kiitwacho 'Maombi ya Kubadilisha' (Transforming Prayer). Katika maombi, sisi huwezesha mazungumzo kati ya Yesu na mtu aliye na hitaji. Tunaomba mpaka Yesu apenye na kutimiza sehemu moja au zaidi kati ya zile tano za huduma yake ya LUKA 4:18-19 . Mabadiliko ya kudumu mara nyingi hutokea katika maisha ya mtu.

Betty ni mwalimu mstaafu wa sayansi na nimekuwa na taaluma mbili katika huduma tangu 1986 - kufanya kazi katika huduma za bima na mauzo. Mimi na Betty tumeoana kwa miaka 49 na tuna watoto watatu wazima na wajukuu watatu.

SASA KUTOKA KWA RICHARD: Katika familia yangu, nilikuwa mtoto mkubwa na nilikuwa na dada watatu. Mama yangu alikuwa Mkristo na yeye daima alitupeleka sisi watoto kanisani (wakati baba yangu hakuonyesha kupendezwa). Kupitia ushawishi wake nilizaliwa upya nikiwa na umri wa miaka 16.

Nikiwa katika Chuo Kikuu cha Arkansas, nilikutana na Kathy Franklin na tukaoana tarehe 6 Januari, 1973, nikiwa nimebakisha mwaka mmoja na nusu kabla ya kumalizia chuo kikuu. Jumatatu iliyopita ilikuwa kumbukumbu ya miaka 52 ya ndoa yetu. Mungu alitubariki kwa watoto 5 (wasichana 2 na wavulana 3) ambao wote wameoa mke wa Kikristo, na sasa tuna wajukuu 18.

Kazi yangu ya kitaaluma ilikuwa kuuza bima ya maisha na afya kwa miaka 47, na nilistaafu katika mwaka wa 2021. Katika miaka hiyo ya kazi, katika matembezi yangu ya kiroho na Mungu, nilijifunza umuhimu wa kutoa na "kujiwekea hazina yako mbinguni". Pia katika miaka hiyo, Mungu alituunganisha mimi na Doug na tuliamua kuruka katika huduma ya Yesu kupitia Roho Mtakatifu kulingana na Mafundisho ya Yesu katika YOHANA 14:12a.

Tumemwona Bwana akitenda mambo makuu na ya ajabu, na tumenyenyekezwa kuwa tumeweza kushiriki. Kwa sasa tunafurahi kuona kile Atakachofanya zaidi.

Kuanzia mwaka wa 1987 tumeongoza mafunzo mengi ya siku moja hadi tatu kote nchini Kenya,  baadaye Tanzania, na hatimaye mwaka huu ndani ya Rwanda.

Kusudi letu ni kumuamsha kikamilifu na kumuandaa kila mmoja wa viongozi wa Mungu bora zaidi ili awe tayari:
• Kufanya huduma ya Yesu (**YOHANA 14:12a; LUKA 4:18-19**).
• Kuwandaa watu wote wa Mungu kufanya huduma ya Yesu (**MATHAYO 28:18-20; WAEFESO 4:11-16**).
• Kuukuza na kuudumisha uhusiano wa kina na wa kudumu na Mungu kupitia Yesu Kristo ndani ya Roho Mtakatifu (**Yohana 15:1-17**).
• Kusogeza juhudi za huduma kutoka kwa 'nyongeza' hadi kwa 'kuzidisha' katika uinjilisti, uongozi, mafunzo, na upandaji wa makanisa, na;
• Kufanya maombi kwa ajili yako katika Afrika Mashariki unapomtumikia Mungu kwa uaminifu katika magumu na mazingira yenye changamoto.

Tunaona mafanikio yako maishani na tija yako katika huduma kama thawabu yetu kwa ajili yetu kuunga mkono juhudi zako kutoka mbali.

Katika Mwaka wa 2025 mawazo yetu ni
• Kuendelea na mafundisho ya kila wiki ya 'Africa Post'.
• Kufungua tovuti ambayo itakupa ufikiaji wa Machapisho ya zamani na huduma zingine na nyenzo za mafunzo (zinakuja hivi karibuni!).
• Kuendesha matukio ya mafunzo kupitia mtandao wa ZOOM (na ana kwa ana jinsi Mungu atakavyowezesha), na
• Kuratibu rasilimali na juhudi miongoni mwa viongozi mbalimbali wa Kikristo na huduma ili kuimarisha uinjilisti wa kila mtu na juhudi zake za upandaji wa makanisa.

Mwaka ujao unaahidi kuwa mwaka wa mabadiliko makubwa, fursa mpya, na hatari kubwa ulimwenguni. Pia tunatarajia mwaka wa 2025 kuwa mwaka ambapo Mungu Atajionyesha upya, kwa nguvu, na kwa njia za kushangaza.

Tunapokaa kuzingatia maonyesho ya Mungu, tutasimama na tutashinda kile ambacho Ataweka mikononi mwetu kufanya.

Ninamalizia kwa kusema kwamba mimi na Richard tumebarikiwa kupindukia na Mungu na pia na wengi wenu kwakuwa tumepata fursa ya kuwa sehemu ndogo ya maisha yako. Tunamshukuru Mungu na kukushukuru hata wewe -  asante kwa upendo wa thamani wa kuwa sehemu ya kile Anachofanya katika Afrika ya Mashariki.

Heri ya mwaka mpya!

*Douglas* Mwandishi *Richard* Mhariri

*JK* Kiswahili Tafsiri *Noella* Kiryarwanda Tafsiri

Ni wako Douglas and Richard
Huduma za 'Jesus Ministries International'.

